**KISWAHILI**
**KIDATO CHA 3**

**KARATASI YA PILI**

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Kauli ya wahenga ilinena kuwa, jambo usilolijua ni usiku wa giza. Maneno haya yalienda sambamba na maisha ya Mhepa, mwanafunzi aliyependa kutoroka shule

Mitihani ilikuwa inapiga hodi na kila mwanafunzi alikuwa ametulia darasani **akibukua.** Mara upepo mwanana ukapeperusha sauti ya muziki kutoka mbali. Masikio ya Mhepa yakaunasa mdundo huo na kumtia mshawasha wa kutoroka. "Kiranja, mimi sijisikii vizuri. Naomba nirudi bwenini," alidanganya. Kiranja alimkataza. Alivifahamu vituko vyake barabara. Alimjua kama kijana mtoro. Mara ngapi alipewa nasaha na walimu! Mara ngapi alipewa adhabu! Kwa kweli Mhepa alikuwa kigego. Waswahili walisema sikio la kufa halisikii dawa. Roho haikumpa kuketi darasani. Alinuka mara kwa mara, ungedhani amekalia kaa la moto. Mara huyo! Akachomoka nje kama mshale wa msasi na "Potelea mbali" alitamka.

Magoma yalilia du! du! du! Huku watu wakidemka ungedhani wamepandwa na pepo. Mhepa alikuwa amebadilika. Ungeambiwa ni mwanafunzi ungekataa. Aliifunga suruali yake ya dangarizi nusu makalioni ungedhani ingemvuka wakati wowote. Alivaa fulana iliyomshika mwili na kumbana. Kipuli kimoja kilining'inia sikio moja na mkufu mkubwa ulilewalewa shingoni. Alishikwa na madadi kwa mdundo wa muziki kiasi cha kujirusha juu na chini mithili ya nyati akimbiaye kwenye mbuga ya Tsavo. Hakuhisi uzito wa mibunda ya soli ya mijiatu aliyovumbika viguu vyake vyembamba kama fito. Pia alibeba shanta.

Mhepa hakujua kuwa dunia mti mkavu, kiumbe usiulemee. Katika rukaruka zake alimkanyanga bwana mwingine mfupi kama nyundo **aliyetutumka misuli.** Yule bwana hakumchelewesha. Alimwangushia sumbwi moja la nguvu kifuani. Kisogo cha Mhepa kikaramba sakafu. Akaona giza la ghafla. Alipofungua macho aliona **vimulimuli**. Umati wa watu ulitumbuizwa kwa sinema hiyo ya bure. Wengi walishangazwa kumuona kibete akimwangusha kijana mwenye tambo kubwa. Labda hawakusomeshwa methali kuwa, "Chura huweza kumuua tembo."

Haikupita hata nusu dakika walinda usalama walifika. Alizolewa pale chini akanyanyuliwa juujuu na kutupwa kweye gari lao. Alifikishwa kituo cha polisi na kuanza kuhojiwa. Mhepa alijibu kijeuri, "Mimi sitajibu maswali yenu." Polisi mmoja nusura ambubute kwa kirungu kama si kuzuiwa na wenzake. Alikiachilia kirungu na kumwahi kofi moja lililomwangusha mtoro huyo upande wa pili. Alipoinuka **alitanabahi** kuwa 'usiyavuke maji usiyoweza kuyaongelea.' "Mimi ni mwanafunzi msiniue jamani. Nasoma shule ya Kigogota. Sare zangu za shule ndizo hizi," alilia huku akifungua shanta yake kuwaonyesha polisi.

Kila asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia. Mhepa alilala seli. Mwalimu wa zamu aliyekuwa akimtafuta pamoja na bawabu wa shule walipigiwa simu na askari usiku huo kufahamishwa alikokuwa Mhepa. Hapo ndipo roho ya mwalimu ilipotulia. Asubuhi Mhepa alipelekwa shuleni na kukabidhiwa Mwalimu Mkuu.

"Hata msingemleta kwangu, mngemchukulia hatua za kisheria. Tulikuwa tumeandikiana mkataba kuwa akifanya kosa la kutoroka tena afukuzwe shule," **alifoka** Mwalimu Mkuu. "Sitarudia tena, nisamehe," alilia Mhepa huku shavu limefura kama andazi moto.

"Ngojea barua uende ukamwite mzazi," alijibu Mwalimu Mkuu. Mhepa aliposikia jina la mzazi alizidi kilio kwani Sajini Mkwara hakuwa mzazi **wa kuonyeshwa meno**. Hasira zake zingeivunja bilauri kwa kuikodolea macho tu.

**MASWALI**

a) Upe ufahamu anwani mwafaka. (alama 2)

Mhepa
Mhepa mtoro
Vituko vya Mhepa.

b) Kwa nini Mhepa alimdanganya kiranja kuwa hajisikii vizuri. (alama 2)

Alikuwa amesikia mdundo uliomtia mshawasha wa kutoroka.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(alama 2)

c) Kwa nini hungedhani kuwa Mhepa alikuwa mwanafunzi?

Alikuwa amejibadilisha kwa kuvua sare na kuvaka mavazi mengine. (suruali ya dangarizi, fulana iliyombana, kipuli sikioni na mkufu.)

(alama 2)

d) Ni jambo gani lililotuliza roho ya mwalimu?

Alikuwa amepigiwa simu na askari usiku huo na kufahamishwa alikokuwa Mhepa.

(alama 1)

e) Taja jina la babake Mhepa.

Sajini Mkwara

(alama 2)

f) Eleza maana ya methali ifuatayo kulingana na taarifa.
Sikio la kufa halisikii dawa

Mtu wa kupotoka/kuharibika ni wa kuharibika. Mhepa alipotoka hata ingawa alijaribu kurekebishwa.

(alama 2)

g) Fafanua maana ya msemo huu "Roho haikumpa kuketi darasani"

Hakuweza kutulia darasani

(alama 2)

h) Fafanua maana ya msamiati kama ulivyotumiwa katika kifungu.
i) Akibukua

- Wanafunzi walikuwa wakidurusu/kusoma kwa maandalizi ya mtihani

ii) alitanabahi.

- Alikumbuka

2. **Ufupisho (alama 15)**

Soma makala haya kisha ujibu maswali yafuatayo.

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watalipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya mikaso inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea wakenya mateso.

Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi. Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yanaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesua wafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

**MASWALI**

a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi.( maneno 60 – 70) (alama 7)

**Matayarisho**

(i) Ugaidi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu.
(ii) Wakenya wasio na makosa huteswa na kuuawa kinyama na watu wasio na utu.
(iii) Magaidi yamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa.
(iv) Magaidi watalipia damu ya wananchi wasio na makosa.
Ugaidi si vita vya kidini - hakuna dini inayoamini kumuua binadamu asiye na makosa.
(vi) Polisi wanapaswa kubuni njia mwafaka za kusaka wahalifu.
(vii) Magaidi huendeleza uhalifu polisi wanapokuwa wakifanya kazi yao

**Nakala safi**

zozote 7 x 1 = 7
Utiririko 1 = $\frac{1}{8}$

b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6)

**Matayarisho**

(i) Hali inayowaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.
(ii) Misako imeishia kunasa raia wasio na makosa na kurundikwa kwenye seli.
(iii) Wanapoachiliwa huwa tayari wameteseka.
(iv) Huu ni ukiukaji haki za raia.
(v) Pia mbinu hii ni hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi huku majambazi wakiendelea kufanya uhalifu.
vi) Polisi wanafaa, kubuni njia mwafaka za kusaka wakora.
(vii) Kuwepo kwa ushirikiano baina yao na majasusi na raia.

**Nakala safi**

(viii) Watapata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Tambua sifa mbili za sauti ifuatayo. (alama 2)

/sh/- Kikwamizo
- sauti ya kaakaa gumu
- sauti sighuna/hafifu.

b) Andika neno lenye muundo ufuatao. (alama 2)
Irabu, konsonanti, konsonanti, irabu

imba, onyo, umbo, omba,

c) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (alama 3)
Niliyempikia

Ni – li – ye – m – pik – i – a
Ni – nafsi; li – wakati; ye – rejeshi; m – kitendwa; pik – mzizi; i – kauli; a – kiishio

d) Onyesha aina za vielezi katika sentensi zifuatazo. (alama 3)
i) Barabara ndefu ilisakafiwa barabara
Namna halisi

ii) Kiplangat alianza kula alipoambiwa angeenda kumlaki mgeni kituoni.
Mahali

iii) msichana Yule alizungumza kitausi.
Namna mfanano

e) Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa. (alama 2)
Mwanamke huyu alibeba ndoo hizi hadi sokoni.
Janajike hili lilibeba madoo haya hadi sokoni.

f) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 3)
Maliwa alimwambia Farida kuwa angewatembelea wazazi wao siku hiyo jioni.
"Nitawatembelea wazazi wetu leo jioni," Maliwa alimwambia Farida.
"Nitawatembelea wazazi wenu leo jioni," Maliwa alimwambia Farida.

g) Amrisha katika wingi. (alama 1)
Lala – Laleni!
Kalaleni!

h) Andika sentensi zifuatazo upya ukitumia vinyume vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
i) Nyua hizi zimejengwa hivi majuzi.
Nyua hizi zimebomolewa hivi majuzi.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ii) Mama alijitwika kikapu mgongoni na kuondoka.

Mama alijitua kikapu mgongoni na kuondoka.

(alama 2)

i) Onyesha shadda inapowekwa katika maneno yafuatayo

i) Mwanafunzi – Mwana'funzi

ii) Alhamisi – Alha'misi

(alama 3)

j) Huku ukitoa mifano, onyesha matumizi matatu ya Kistari kifupi.

(i) Kuandika tarehe – 20-10-2022
(ii) Kutoa maelezo zaidi – Dhamira-lengo la mwandishi.
(iii) Kutenga silabi katika neno – Mwa-na-fu-nzi
(iv) Kutenga muda – 1980-1984, Saa 4.00 – Saa 4.30.
(v) Kuonyesha neno linaendelea katika mstari unaofuata utq-enda
(vi) Kutanguliza mzizi wa neno – -eupe, -zuri, -pi

(alama 4)

k). Kanusha sentensi zifuatayo kwa wingi.

Mvua kubwa inayoyesha itasababisha mafuriko

Mvua kubwa inayonyesha haitasababisha mafuriko

Alilia na kulaani

Hakukulia wala kulaani.

l) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno hili 'paka' (alama 2)

Paka – mnyama anayefugwa nyumbani. Paka amemla panya.
Paka – eneza kitu cha majimaji mf. rangi kwenye kitu kingine. mf. Paka rangi ukutani.

m) Bainisha aina za virai vilivyopigwa mstari. (alama 2)

Mhadhara huo tata ulitolewa jana jioni

Kirai kivumishi | Kirai kielezi

n) Tumia neno '- refu', kama; (alama 3)

i) Nomino

Alijenga jumba lenye urefu wa ghorofa tatu.

ii) Kiwakilishi

Ndefu imejengwa mjini.

iii) kivumishi

Nyumba ndefu imejengwa mjini.

o) Changanua kwa mistari. (alama 2)

Usiuchukue ushauri huu hivi hivi

T S KN V E

au

S – KN+KT
KN – Ø
KT – T+N+V+E

T – usiuchukue
N – ushauri
V – huu
E – hivi hivi

(Tuza njia yoyote ile)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

p) Eleza maana nne zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 4)
Kuvuza alimpigia Oliech mpira

- Alipiga mpira kwa niaba ya Oliech.
- Alipiga mpira ukaelekea kwa Oliech.
- Alitumia mpira kumpiga Oliech.
- Alimpiga Oliech akitumia mpira.

**Isimu jamii (ALAMA 10)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

A: Bwana mdogo, leo wajisikiaje?
B: Nafeel poa, Leo niko better kuliko jana.
A: Sawa, endelea kutumia hizi dawa hadi uzimalize.........................

a) Tambua sajili hii. (2mks)

Sajili ya kituo cha afya/zahanati/hospitali.

b) Eleza sifa nane zinazohusishwa na sajili hii. (alama 8)

(i) Huwa na msamiati maalum wa matibabu mf. daktari, mgonjwa, dawa, lab, x-ray.
(ii) Huwa na maswali na majibu - Daktari anapotaka kujua kiini cha ugonjwa.
(iii) Lugha huwa ya heshima/adabu.
(iv) Lugha ya matumaini, matumiwa na daktari kwa mgonjwa
(v) Ni lugha inayoeleweka na wagonjwa wa kila tabaka.
(vi) Lugha ya ishara, mgonjwa anapoonyesha daktari anakoumia
(vii) Lugha huchanganya ndimi. Mfano Lab, x-ray, test.
(viii) Matumizi ya tarakimu. Mfano Meza tembe 1X3 kwa siku.

(8 x1 = 8)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes